

# Watu 200,000 watoa maoni mitaala mipya

**Va Aveline Kitomary**

**W**IZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mesema tayari watu zaidi 200,000 wameshatoa naoni huku ukurasa wa naoni ukitarajiwa ku-ungwa rasmi wiki ijayo Mei 31, 2023.

Aidha, mtaala mpya wa elimu unatarajiwa kuanza kutekelezwa Januari, 2024

ambapo miongoni mwa mapendekezo yaliyowasilishwa ni pamoja na elimu ya lazima kuwa miaka 10 huku elimu ya msingi kuishia darasa la sita na elimu ya sekondari kwa miaka minne.

Akizungumza Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi wa kamati ya Ushauri wa Kiviwanda ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), ambayo itashauri

kuhusu mitaala, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Profesa James Mdoe alisema katika kukuza sekta ya elimu ya juu serikali imefanya juhudi za dhati kuanzisha na kutekeleza Mradi wa Elimu ya Juu (HEET).

“Kupitia mradi huu, serikali itaboresha mitaala, rasilimali-watu na mazingira ya kufundishia na kujifunza katika vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu 23

ili mfumo wetu wa elimu ya juu ujikite zaidi katika kutoa elimu ujuzi itakayowafanya wahitimu kuzalisha ajira au kujiajiri,” alieleza.

Aidha, alisema mradi utanzisha kampasi 14 za vyuo vikuu katika mikoa ambayo ilikuwa haina taasisi za elimu ya juu zitakazokuwa zinalelewa na vyuo vikuu kamili vinavyotekeleza mradi huo.

Alisema kwa MUHAS kuna mradi wa kukara-

bati na kujenga kampasi za Mloganzila na Kigoma, kuboresha miundombinu ya kujifunza na kufundishia, kuhuisha au kuandaa mitaala, kusomesha watumishi, kuweka miundombinu ya kisasa ya TEHAMA na kuweka mifumo ya kidijitali kwa ajili ya kufundishia na utawala pia.

Alifafanua kuwa Mradi wa HEET utaongeza idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu

nchini kwa asilimia 30 katika maeneo 14 ya kipaumbele kwa uchumi wa kati wa viwanda.

“Ili kutekeleza agizo hili, kupitia HEET wahitimu wa Elimu ya Juu wanaokusudiwa kuongezeka watajikita katika elimu ujuzi ambapo hadi sasa tuna asilimia 3.5. Nni muhimu tuwaongeze hadi kufikia asilimia 12 wanaohitajika katika uchumi wa kati wa viwanda,” alisema.